**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI**

**SHULE YA SEKONDARI UFUNDI MTWARA**

**Namba za Simu**
**Makamu Mkuu wa Shule 0717115098**
**Patron 0712280710**
**Matron 0713943566**
**Mkuu wa Shule 0713830862**
**Shule ya Sekondari UFUNDI MTWARA**

**S.L.P104**

**Tarehe ..............**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UFUNDI MTWARA ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI MKOA WA MTWARA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **UFUNDI MTWARA** ipo umbali wa Kilometa 06 KaskaziniMagharibi mwa Mji wa MTWARA. Usafiri wa **Bodaboda au Bajaji** kutoka Stendi Kuu ya Mabasi unapatikana kwa nauli ni Shilingi 2,000/= kwa Bodaboda au 3,000/= kwa Bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe .../.../2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..../..../2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe .... /.../2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

**Sare ya shule**

a) Sare ya shule

**Wasichana**; Sketi(2) zenye Marinda ya kawaida Rangi ya Dark-blue- urefu ifikie **kifundo cha miguu**, Mashati mawili meupe Mikono mirefu, Tai rangi ya Dark – blue, Viatu vyeusi vya Kamba na Soksi nyeupe

Vazi la Hijab rangi nyeupe(Juba) lifike kwenye **kifundo cha mkono** na nusu kanzu yake **ndefu**.

**Wavulana;** Suruali mbili Nyeusi zenye marinda mawili au matatu, Mashati mawili meupe Mikono mirefu, Tai rangi ya Nyeusi, Viatu vyeusi vya Kamba , Soksi nyeupe na Mkanda mweusi usio na mapicha.

b) Sare ya michezo:

**Wasichana**, Tracksuit mbili za blue( **zisizobana**) na Raba za michezo.

**Wavulana,** Bukta mbili na Tracksuit mbili za blue na Raba za michezo**.**

c) Sweta rangi ya Dark- blue moja.

d) Nguo za kushindia (shamba dress):

**Wasichana**; T-Shirts Mbili zenye kola (Form Six) rangi ya kijani.
,Gauni au sketi mbili rangi ya kahawia (brown)

**Wavulana ;** T-Shirts Mbili zenye kola (Form Six) rangi ya kijani.
Suruali mbili rangi ya kahawia (brown)

**NB: 1. Kwa kuwa kuna tatizo la wazazi /walezi wengi kukosea rangi,malighafi,mashono (mtindo) hivyo kupelekea T Shirt na sare na nguo za kushindia kuwa tofauti na zile zinazohitajika shuleni,mzazi/mlezi unashauriwa zije kushonewa jirani na hapa shuleni.**

### 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari (kaunta book) zisizopungua 10
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatashwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro la futi 2 na nusu
vii. Mashuka Jozi 2, ( jozi 1 ya pink na jozi 1 ya bluu)
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 wa ndani na nje na dawa ya chooni lita 5.
xii. Laboratory coat rangi nyeupe.
xiii. Aje na bima ya afya. Kama hana mzazi/mlezi anashauriwa aje na kiasi cha fedha tsh 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya.( NHIF).

## 2.2 Michango mbalimbali.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**ACCOUNT YA KULIPIA NI -NMB 70601200070-MTWARA TECHNICAL SEC SCHOOL**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia **ratiba ya shule wakati wote**;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI UFUNDI MTWARA**
**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**
**Riyadh Kadhi**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mwandamizi Malezi ……0787425666 AU 0713768821**
- **Mwandamizi Taaluma …0784225245**
- **Makamu Mkuu wa Shule...0717115098 AU 0684369731**
- **Mkuu wa shule ……0713830862**

**MEDICAL EXAMINATION FORM (HATI YA DAKTARI)**

Mtwara Technical Secondary School,
P.O.Box 104,
MTWARA.
Date................................

TO THE MEDICAL OFFICER**,**

NAME: ………………………......................................................

Please examine the above named as to his /her fitness for further education at Mtwara Technical Secondary School in the areas;

| | **NORMAL** | **NOT NORMAL** |
|---|---|---|
| EYES | | |
| EARS | | |
| RESPIRATORY SYSTEM | | |
| GIT | | |
| CVS | | |
| URINE/STOOL | | |
| VDRL | | |
| STOMACH ULCERS | | |

RIYADH.A.KADHI.

**HEADMASTER**

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by the Medical Officer)

I have examined the above named consider that he/she is.........................................................

.......................................................................take up the studies.

Date…………………. Name and signature ....…………………….............................

Station………………. Designation…………………………………

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Fomuya maelekzo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

Mimi ............…………………………...………….. niliyechaguliwa kujiunga na Kidato cha .................. mwaka ............... nimesoma na kuyaelewa maelezo ya kujiunga na Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara na ninaahidi kwamba:-

i. Nitafuata na kutekeleza Sheria na Kanuni zote za Shule hii.
ii. Naahidi kutoshiriki katika migomo ya aina yoyote, fujo na makosa ya Jinai.
 Endapo nitaenda kinyume Sheria na Kanuni zote za Shule hii na kushiriki katika migomo ya aina yoyote, fujo na makosa ya Jinai, HATUA KALI ZA KINIDHAMU zichukuliwe dhidi yangu.

Tarehe………………….. Sahihi……………………………..

a) Fomu ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria , kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule(Ijazwe na Mzazi/Mlezi Mwenyewe);

Mimi………………………..............................ambaye ni mzazi/mlezi wa kijana wangu aitwae ……………….................................…nakubaliana na Sheria na Kanuni za Shule. Nitayakubali na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule hii.

Tarehe…………………… Sahihi…………………………

b) Picha NNE za wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

Picha ya mzazi(baba)/Mlezi wa kiume Picha ya mzazi (mama)/Mlezi wa kike

Jina: ........................................... Jina: ..................................................

Namba ya Simu ………………………..Namba ya simu………………………………..

Picha ya Ndugu wa Karibu

Jina: ..........................................

Namba ya Simu ………………………..

Picha na Ndugu wa Karibu

Jina: ................................................

Namba ya simu……………………………….

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

## VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI HUSIKA

**Biology:**

1. Biological Science
2. Understanding Biology
3. Functional Approach

**Chemistry:**

1. Principal of Chemistry
2. General with Physical Chemistry (APE Network)
3. Organic and Inorganic Chemistry (Mzumbe Project).

**Physics:**

1. Principles of Physics Class XI and XII
2. Advanced Physics by Nelkon & Parker 5th, 6th and 7th Edition
3. A-level Physics By Rodgers Muncaster
4. Understanding Physics

**Advanced Mathematics**

1. Pure Mathematics 1 & 2 by J.K. Back House
2. Understanding Mathematics
3. Advanced Mathematics 1 &2 by S. Chands
4. Mathematics : The core Course for A – level By Bostock
5. Mathematics By C.J.Tranter

**Geography**

1. Geography for Secondary Schools Form Five By TIE
2. An Integrated Regional Studies on Human and Economic Geography By D.T. Musabila
3. Geography , an integrated Approach by David waugh
4. Comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School By D.T. Musabila
5. Physical Geography, A landscape Appreciation by Mcknight's

**General studies**

1.General Studies Alive. A Straight Forward General Studies For High School and University Students By Zisti Kamili,2017)

2.Understanding General Studies For Advanced level By Joannes Bigirwamungu,Sospeter M,Deogratias, 2018)